

Swald Amiri,

S.L.P 1331,

Mwanza.

Aprili 1, 2020.

Msajili,

Baraza la Famasii, Tanzania

S.L.P 1277

Dodoma

Ndugu,

YAH: NOTISI YA KUSITISHA USIMAMIZI WA GLOBAL PHARMACEUTICALS, MWANZA.


Mimi, Swald Amiri, ni mfamasia niliyesajiliwa na Baraza lako na kupewa namba ya utambulisho PIN 0100877. Mimi ndiye mfamasia msimamizi wa Global Pharmaceuticals LTD iliyopo jijini Mwanza, Wilayani Nyamagana, mtaa wa Bantu.

Kwa barua hii, nakujulisha rasmi kwamba ninasitisha usimamizi huo kwa kutoa notisi ya siku (90) kuanzia tarehe ya usainiwaji wa barua hii (Aprili 1, 2020). Kwa kipindi hiki cha notisi, nitaendelea na majukumu na wajibu wangu kama yalivyoanishwa kwenye sheria na kanuni za Pharmacy Act, 2011.

Mimi na mmiliki wa Global Pharmaceuticals LTD tunajadili juu ya jinsi atakavyonilipa posho yangu ya usimamizi ya kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020 ndani ya kipindi hiki cha notisi kwani hajafanya hivyo kwa kipindi tajwa.

Nitahakikisha taratibu zote za kitaaluma zinafuatwa katika kipindi hiki chote cha notisi kama zilivyoanishwa kwenye sheria tajwa hapo juu pamoja na maboresho yake na kanuni zake.

Wako katika ujenzi wa Taifa,



Swald Amiri (0766283006).

Nakala: Mh. Constantine Kanyasu

Mkurugenzi,

Global Pharmaceuticals LTD

Mwanza.

Swald Amiri,

S.L.P 1331,

Mwanza.

Juni 29, 2020.

Msajili,

Baraza la Famasi, Tanzania

S.L.P 1277

Dodoma.

Ndugu,

**YAH: MWISHO WA NOTISI YA SIKU 90 JUU YA USIMAMIZI WA GLOBAL PHARMACEUTICALS LTD,
MWANZA.**

Rejea barua yangu ya tarehe 1 April 2020 yenye kichwa cha habari "Notisi ya kusitisha usimamizi wa Global Pharmaceuticals LTD, Mwanza".

Mimi Swald Amiri ni mfamasia niliyesajiliwa na Baraza lako mwenye PIN 0100877. Napenda kukujulisha kwamba notisi niliyoitoa ya siku 90 inaisha leo, hivyo kukujulisha rasmi kwamba mimi Swald Amiri sio msimamizi tena wa Global Pharmaceuticals LTD iliyopo Kitalu Na. 62, Mtaa wa Bantu, Manispaa ya Nyamagana na Mkoani Mwanza. Yenye Facility Identification Number (FIN) 1903010312.

Kama nilivyoonyesha kwenye barua yangu ya awali, mmiliki wa Famasi tajwa hajanilipa posho yangu tangu Julai 2019 (aliingiza 500,000 pekee Februari 2020) hadi sasa mbali nakukubaliana kuwa na 'payment plan' kwenye kipindi cha notisi.

Kwa barua hii naambatanisha nakala halisi (Original Certificate) ya Premise Registration Certificate na Business Permit kama ilivyo takwa la miongozo kwani katika kipindi cha notisi mmiliki alianza taratibu za kumaliza shehena iliyokwepo ili kuifunga famasi baada ya notisi kuisha na kuendelea na biashara nyingine.

Kwa barua hii napenda kukujulisha rasmi kwamba mimi sio msimamizi tena wa Global Pharmaceuticals LTD iliyopo Mwanza kuanzia kesho June 30, 2020 na kumwelekeza mmiliki kutofanya biashara ya Mfamasia bila kibali cha baraza lakini pia kufuta bango linaloonyesha hivyo.

Wako katika Ujenzi wa Taifa,



Swald (0766283006)

Nakala: Mh. Constantine Kanyasu (MB)

Mmiliki, Global Pharmaceuticals LTD

Swald Amiri

S.L.P 9081

Dar es Salaam

Machi 15, 2025.

Msajili,

Baraza la Famasi

S.L.P

Dodoma.

YAH: KUTOA ILANI YA KUSITISHA USIMAMIZI WA FAMASI

Rejea barua yako yenye Kumb. Na. CA.313/329/01E/60 ya Machi 10, 2025 yenye somo tajwa hapo juu.

Napenda kukufahamisha kwamba mimi Swald Amiri mwenye namba ya usajili wa baraza lako PIN: 0100877 ni kweli nilikuwa msimamizi wa Famasi ya Global Pharmaceuticals LTD iliyokuwa na usajili FIN: 0100901 iliyokwepo mtaa wa Bantu, Manispaa ya Nyamagana , Jijini Mwanza. Kwasasa nipo kikazi Jijini Dar es Salaam kama nilivyolijulisha Baraza lako kwenye taarifa zangu zakuhuisha Leseni yangu kwa mwaka 2025.

Hata hivyo napenda kukufahamisha kwamba nilishasitisha USIMAMIZI wa Famasi tajwa (Global Pharmaceutical LTD) tangu JULAI 01, 2020 na kulitambulisha na kuwasilisha nyaraka zote stahili kwa Baraza lako kupitia Ofisi ya Baraza kanda ya Ziwa. Nilitoa notisi ya siku 90 mnamo April 2020 na barua yakusitisha usimamizi rasmi mnamo Juni 2020 kwako kupitia Ofisi hio ya kanda na taratibu zote zakuifunga Famasi hio zilifuatwa.

Kwa barua hii naambatisha nakala za notisi ya siku 90 pamoja na barua ya usitishaji huo. Napenda kukufahamisha pia kwamba kwasasa sisimamii Famasi yeyote hapa nchini na kama kuna mmiliki yeyote anayetumia jina na/au leseni yangu, naomba Baraza lako lichukue hatua stahiki kwa mmiliki huyo.

Naomba kuwasilisha,



Swald Amiri.

Nakala: Mratibu wa Famasi – Kanda ya Ziwa.